

Oktoba 16, 2019

Kijarida cha Mountain View

Ujumbe wa Mwalimu Mkuu

Ninataka kuwashukuru wale waliokuja katika mkutano wetu wa Baraza la Jamii ya Shule Ijumaa iliyopita. Sauti za wazazi waliojali walichangia ili kufanya shule yetu kuendelea kuwa kuu na kuchangia katifa kuifanya iwe kuu hata zaidi. Tunashukuru mwa mchango na uwekezaji wako.

Maonyesho ya Kutisha ya Halloween

Tunafurahi kutangaza Fair ya Halloween ya Scare ambayo itafanyika Ijumaa, Oktoba 25 kutoka 3:00 hadi 6:00 p.m. katika Kituo cha Kujifunza Jamii. Kutakuwa na uchunguzi wa kiafya, rasilimali za afya za jamii, shughuli za watoto, kibanda cha kupigwa picha, na vitisho vya kupata peremende. Mojawapo ya hali za kufurahisha za tukio hili ni kwamba wewe na familia yako mnaweza kuja kupata chanjo za homa bila malipo! Chanjo hizi zitapatikana bidhaa zikipatikana kati ya 12:00 na 6:00 p.m. Lazima wapokeaji wa chango wawe na umri wa angalau miaka misaba. Tunahimiza kila mtu kushiriki. Kuwa mgonjwa hugarimu familia pesa, muda, na wasiwasi. Epuka magonjwa nyumbani mwako kwa kupata chango. Tunataka kushukuru Walgreens, Wakfu wa Elimu wa Salt Lake, na Shirika la Afya ya Jamii la Utah kwa kufanya tukio na chanjo hizi ziwezekane.

Shughuli Inayopendekezwa ya Kuongeza Kiwango cha Kuzingatia Hisia za Wengine cha Mtoto Wako

Jarida la wiki iliyopita lilipendekeza shughuli ya kusaidia kuwafunza watoto kuwa na huruma. Dkt. Michele Borba anapendekeza kuwaalika watoto waweze kujifikiria wenyewe wakipitia hali ya maisha ambayo hao wenyewe hawajawahi kupitia awali, na kisha washiriki mawazo yao kwa kuchora picha au kuandika kuhusu walichofikiria.

Itakuwa pia wazo nzuri kwa watoto wetu kupitia hali hizo kwa halisi. Kwa mfano tunaweza kuwapeleka watoto wetu kuzuri nyuma ya watu wasiokuwa na makao, watoto wafungwa, au makao ya utunzaji. Mtu anaweza kumpa mtoto uzoefu wa kuwa na ulemavu kwa kumziba macho kwa kitambaa, kumkalisha katika kiti cha magurudumu, au kutotumia sauti yake kwa muda. Baada ya uzoefu huu, itakuwa vizuri kwa mtoto huyo kuzungumzia au kuandika kuhusu uzoefu huo, kwa kumuuliza kama maoni yake ni sawa au tofauti na alivyofikiria. Dkt. Borba anapendekeza unaweza hata kurudi na ujitolee na mtoto wako ili aweze kuwa na mtazamo tofauti.



Matukio Yanayokuja

Alhamisi, Oktoba 17

Hakuna Shule, Mapumziko ya Majira ya Kupukutika kwa Majani

Ijumaa, Oktoba 18

Hakuna Shule, Mapumziko ya Majira ya Kupukutika kwa Majani

Jumatatu, Oktoba 21

Hakuna Shule, Mapumziko ya Majira ya Kupukutika kwa Majani

Ijumaa, Oktoba 25

Chanjo ya Homa ya Bila Malipo, 12:00-6:00,

CLC ALHAMISI, Oktoba 31

Paredi ya Halloween, 1:30

Mkutano wa Ushauri kwa Wazazi

Kila asubuhi ya Ijumaa wazazi wana nafasi ya kujifunza kuhusu mfumo wa elimu, kukutana na kitivo na wafanyakazi wa shule, na kujadili masuala muhimu katika uzoefu wa watoto wao shuleni. Tunakualika ufike siku ya Ijumaa na uwe sehemu ya majadiliano haya. Tunakutana saa 8:15 katika Kituo cha Masomo cha Jumuiya, Chumba 182. Ikiwa unahitaji msaada kukipata, wafanyakazi wetu katika ofisi watakusaidia kupata maelekezo ya njia sahihi. Natumai kukutana nawe!

Baraza la Jumuiya ya Shule

Baraza la Jumuiya ya Shule (SCC) itakutana kila mwezi katika CLC. Mikutano ya SCC ni wazi kwa umma.

Fuata au Uwe Rafiki wa Shule ya Mountain View kwenye Mitandao ya Kijamii

Facebook: @MountainViewSLC.

Twitter: @mtviewlibrary.

Tunatarajia kuwa utatufuata, na tunatumai kuwa utaalika jamaa na marafiki ili kutufuata, pia.

Masomo ya Kituo cha Mafunzo cha Jumuiya

Kituo chetu cha Mafunzo cha Jumuiya kinatoa masomo mengi kwa ajili ya wanafunzi na watu wazima. Tafadhali tembelea ofisi za Kituo cha Kujifunza Jumuiya ili ujipatie kalenda husika. Mtu yeyote wa jumuiya yetu anakaribishwa kujiandikisha na masomo.

MV LIMB Newsletter 101619 SWAHILI 2019-10-16

Hakuna mwajiriwa au mwanafunzi wa wilaya atakayebaguliwa katika ajira au programu au shughuli yoyote ya wilaya kwa misingi ya umri, rangi, ulemavu, jinsia, taarifa za vinasaba, utaiifa, ujauzito, mbari, dini, utambulisho wa kingono, au hali ya ustaafu. Wilaya imeathamiria kutoa ufukio sawa na fursa sawa katika programu zake, huduma na ajira ikiwemo sera zake, michakato ya malalamiko, ufikaji wa programu, matumizi ya huduma za wilaya, malazi na masuala mengine ya Fursa Sawa za Ajira. Wilaya pia inatoa ufukio sawa kwa huduma za wilaya kwa makundi yote ya vijana yaliyoorodheshwa katika Title 36 ya Sheria ya Marekani, ikiwemo makundi ya skauti. Mtu afuataye amechaguliwa kushughulikia maaulizo na malalamiko kuhusiana na masuala ya ubaguzi, unyanyasaji, na ulipizi ulio kinyume na sheria: Tina Hatch, Uthi na Uchunguzi, 440 East 100 South, Salt Lake City, Utah 84111. (801) 578-8388. Unaweza pia kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Kiraia, Denver, CO, (303) 844-5695.

Tovuti: mountainview.slcschools.org Simu: 801-974-8315

Ukurasa wa 1 kati ya 1